TANGAZO LA SERIKALI Na. 32 la tarehe 12/1/2024

# SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA, (SURA YA 290)

---

## SHERIA NDOGO

---

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA HUDUMA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogohii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Rombo;

"kipindi maalum cha hesabu" maana yake ni muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara kwa Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi

Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza kazi za Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hii;

"mlipa ushuru wa huduma" maana yake ni taasisi, kampuni, tawi la kampuni au mfanyabiashara mwenye leseni anayefanya shughuli zake katika eneo la Halmashauri;

"ushuru wa huduma" maana yake ni ushuru unaotozwa na kukusanywa na Halmashauri kutoka kwa kampuni, tawi la kampuni au mfanyabiashara yeyote mwenye leseni ya biashara ambaye mauzo yake kwa mwaka ni zaidi ya shilingi milioni nne kutokana na huduma anazopata na kutumia miundombinu ya umma inayomuwezesha kufanya biashara katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri..

Ushuru wa huduma

4.-(1) Halmashauri itakusanya na kutoza ushuru wa huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kutoka kwa kila kampuni, tawi la kampuni, taasisi ya biashara, mfanyabiashara yeyote mwenye leseni ya biashara na mtoa huduma yeyote yule kwa kiwango kisichozidi asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) kutokana na uzalishaji wa bidhaa, kazi na huduma zinazofanyika au kutolewa ndani ya eneo la Halmashauri ukiondoa kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo

ya (1), Halmashauri itatoza na kukusanya Ushuru wa Huduma kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii kutoka kwa wafanyabiashara wenye leseni za biashara ambao wameshindwa kutunza kumbukumbu za kibiashara.

Wajibu wa mlipa ushuru

5.-(1) Kila mlipa ushuru wa huduma atakuwa na wajibu wa-

(a) kulipa ushuru wa huduma kwa kiwango kilichoainishwa katika Sheria Ndogo hii;
(b) kuwasilisha taarifa sahihi za mauzo ya kila mwezi endapo anawasilisha taarifa za hesabu za mauzo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.
(c) kuwasilisha hesabu sahihi na za kweli;
(d) kuwasilisha nyaraka, maelezo au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa kwa Halmashauri katika muda uliowekwa;
(e) kutunza kumbukumbu, vitabu au hesabu; na
(f) kuonyesha kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya uchunguzi.

(2) Kila mlipa ushuru wa huduma atatakiwa kulipa ushuru wa huduma si zaidi ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuwasilisha taarifa za mauzo ya kila mwezi.

(3) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (2), Halmashauri inaweza kukubaliana na mlipa ushuru wa huduma utaratibu wa kulipa ushuru huo.

(4) Kila mlipa ushuru atatakiwa kuwasilisha kwa Halmashauri hesabu za mwisho katika kipindi cha miezi mitatu tangu kumalizika kwa kipindi cha hesabu.

(5) Iwapo mlipa ushuru hajawasilisha hesabu za mwisho kwa mwaka wa fedha husika

na ametakiwa kufanya hivyo kwa notisi ya siku thelathini, Mkurugenzi anaweza kwa kadri atakavyoona inafaa, kukadiria kiwango cha hesabu za mlipa ushuru huyo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(6) Ushuru uliofanyiwa tathimini kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, utalipwa katika kipindi cha siku thelathini tangu tarehe ya tathmini.

(7) Iwapo mlipa ushuru hajawasilisha majumuisho ya hesabu zake kwa mwaka wowote wa mapato, na endapo Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa anaona kwamba mlipa ushuru huyo ana wajibu wa kulipa ushuru kwa mwaka huo, anaweza kwa kadri atakavyoona, kukadiria kiwango cha hesabu za mlipa ushuru huyo, isipokuwa tathmini hiyo haitaathiri wajibu wowote wa mlipa ushuru anayostahili kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kwa kushindwa kwake kuwasilisha hesabu hizo.

Mamlaka ya Mkurugenzi

6.-(1) Endapo mlipa ushuru wa huduma anayetakiwa kuwasilisha taarifa ya mauzo chini ya Sheria Ndogo hii atashindwa kuwasilisha taarifa sahihi za mauzo kwa wakati, Mkurugenzi anaweza kutoa notisi ya kumtaka mlipa ushuru wa huduma kuwasilisha taarifa hiyo ndani ya siku thelathini kuanzia tarehe ya kutolewa kwa notisi.

(2) Mkurugenzi anaweza kumtaka kwa maandishi mtu yeyote mwenye taarifa kuhusu mfanyabiashara anayepaswa kulipa Ushuru wa Huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kuwasilisha kwake taarifa hizo.

(3) Mkurugenzi anaweza kumwagiza kwa maandishi afisa mwidhiniwa kuingia kwenye jengo au eneo la taasisi ya kibiashara

au la mlipa ushuru yeyote kwa nia ya kufanya uchunguzi na tathmini ya kumbukumbu za biashara, vitabu vya hesabu na taarifa kwa ajili ya kupata na kujua kiwango sahihi cha ushuru anachotakiwa kulipa.

(4) Mkurugenzi anaweza kumteua Kamishna wa kodi ya forodha au kodi ya mapato kwa ajili ya kutathmini na kukusanya ushuru wa huduma na kuwasilisha kwa Halmashauri kwa lengo la kupata ushuru wa huduma pamoja na madeni yake.

(5) Mkurugenzi kwa taarifa ya maandishi, anaweza kumtaka mlipa ushuru yeyote kuwasilisha hesabu zenye taarifa kamili za shughuli za kibiashara zikionyesha thamani ya kiasi na ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, kutolewa kusambazwa au kuuzwa kibiashara na taarifa ya fedha katika kipindi maalumu kisichozidi siku thelathini tangu tarehe ya taarifa hiyo.

(6) Mkurugenzi, kwa taarifa ya maandishi ya siku saba, anaweza kumtaka mlipa ushuru kuwasilisha kumbukumbu za kibiashara na vitabu vya hesabu kwa nia ya kupata taarifa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini au kukusanya ushuru wa huduma.

Ukokotoaji wa ushuru wa huduma

7. Halmashauri itakokotoa ushuru wa huduma kwa walipa ushuru wa huduma wanaowasilisha taarifa za mauzo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kuzingatia taarifa zinazowasilishwa na walipa Ushuru wa Huduma katika kipindi maalum cha hesabu.

Uteuzi wa Wakala

8. Mkurugenzi anaweza kuteua wakala wa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri na wakala huyo atakuwa na

jukumu la:

(a) kuwasilisha majumuisho ya makusanyo ya ushuru kwa Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa;

(b) kuwasilisha ushuru aliokusanya kwa mujibu wa mkataba.

mamlaka ya afisa mwidhiniwa

9. Afisa mwidhiniwa anaweza-

(a) kupokea na kukubali hesabu za mlipa ushuru na kuzifanyia kutathmini;

(b) kufanya tathmini kuhusu kiwango cha hesabu cha mlipa ushuru endapo hesabu hizo zitakuwa si sahihi;

(c) kukataa hesabu za mwisho na kufanya tathmini kuhusu hesabu hizo iwapo atakuwa na sababu za msingi za kuamini kuwa hesabu hizo siyo sahihi.

Makosa

10.-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kuwasilisha kwa Halmashauri taarifa sahihi za mauzo katika muda ulioainishwa katika Sheria hii;

(b) atawasilisha kwa Halmashauri taarifa zisizo sahihi;

(c) atashindwa kulipa ushuru wa huduma katika muda ulioainishwa katika Sheria hii;

(d) atamshawishi mlipa ushuru wa huduma kukataa au kukwepa kulipa ushuru wa huduma; au

(e) atamzuia Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria hii.

(f) atafanya hesabu za uongo kwa kupunguza au kutoa hesabu zisizokuwa

sahihi kwa Halmashauri au wakala;

(g) atatoa taarifa isiyokuwa sahihi kuhusu jambo lolote linaloweza kuathiri jukumu lake au la mtu mwingine la kulipa ushuru;

(h) ataandaa au atatengeneza au atasababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa vitabu vya uongo vya hesabu au kumbukumbu;

(i) atashindwa kulipa ushuru wa huduma ndani ya muda ulioainishwa katika Sheria hii; au

(j) atashindwa kutunza kumbukumbu yoyote au nyaraka kwa ajili ya ukaguzi.

Adhabu

11. Mtu yeyote atakayetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii na kutiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ushuru anaodaiwa.

______

JEDWALI LA KWANZA

______

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(2))*

VIWANGO VYA USHURU WA HUDUMA

| Na. | Aina ya Biashara au Kiwango cha Ada ya Leseni (Shilingi) | Kiwango cha Kodi ya Huduma (Shilingi) | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | kati ya 10,000/= hadi 20,000/= | 10,000/= | Kwa mwaka |
| 2. | kati ya 30,000/= hadi 40,000/= | 20,000/= | Kwa mwaka |
| 3. | kati ya 50,000/= hadi 90,000/= | 30,000/= | Kwa mwaka |
| 4. | kati ya 100,000/= hadi 150,000/= | 50,000/= | Kwa mwaka |
| 5. | zaidi ya 250,000/= | 150,000/= | Kwa mwaka |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 12)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …… ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Huduma ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ya Mwaka, 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, niko tayari kulipa kiasi cha ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.
Leo tarehe …………………. ya Mwezi …………… Mwaka …………………
Jina: ………………………………………….
Saini: …………………………….

MBELE YA:
Jina: ……………………………………
Cheo: …………………………………….
Saini: ………………………………..
Tarehe: ………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio la Mkutano wa baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 3/3/2023 na Lakiri imebandikwa mbele ya:-

GODWIN JUSTIN CHACHA,
*Mkurugenzi Mkuu,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Rombo*

GILBERT ALEX TARIMO*,*
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Rombo*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (Mb.),
*Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI*,